


**JEDWALI LA MAREKEBISHO LITAKALOWASILISHWA NA MHE. DKT. ASHATU
KIJAJI, WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA, WAKATI WA
KUSOMWA KWA MARA YA PILI KWA MUSWADA WA SHERIA YA UWEKEZAJI
TANZANIA WA MWAKA 2022**

(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 99(10))

Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa mwaka 2022 unarekebishwa kama ifuatavyo:

- A:** Katika Jina refu la Sheria, kwa kuongeza maneno “ulinzi, uvutiaji, uhamasishaji” mara baada ya neno “uratibu”;
- B:** Katika Ibara ya 2(5) kwa kufuta maneno “kitawasaidia wawekezaji wote, bila kujali kuwa Sheria hii inawahu au la” na badala yake kuweka maneno “kitawahudumia wawekezaji wote, bila kujali kuwa Sheria hii inawahu au la, na kuwasaidia”;
- C:** Katika Ibara ya 3-
- (a) kwa kufuta tafsiri ya msamiati “mtaji” na badala yake kuweka tafsiri ifuatayo:
““mtaji” inajumuisha mchango wa fedha taslimu, mitambo, mashine, vifaa, majengo, vipuri, ardhi, hakimiliki na mali nyingine za biashara tofauti na hadhi ambazo hazitumiki katika shughuli za kawaida za biashara na zinazoweza kudumu kwa zaidi ya miezi kumi na mbili;”; na
 - (b) kwa kufuta maneno “maana yake ni” yaliyopo katika tafsiri ya msamiati “mtaji wa kigeni” na badala yake kuweka neno “inajumuisha”;
- D:** Katika Ibara ya 4-
- (a) kwa kufuta maelezo ya pembeni na badala yake kuweka yafuatayo:
“Kuendelea Kuwepo kwa Kituo na malengo”
 - (b) kwa kuongeza mara baada ya ibara ndogo ya (3) ibara ndogo ifuatayo:
“(4) Kituo kitakuwa sehemu ya huduma mahala pamoja kwa wawekezaji na kitakuwa ndicho chombo kikuu cha Serikali cha kuratibu, kuhimiza, kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji Tanzania na kuishauri Serikali kuhusu sera ya uwekezaji na masuala yanayohusiana na hayo.”;
- E:** Katika Ibara ya 5-
- (a) kwa kufuta maelezo ya pembeni na badala yake kuweka yafuatayo:
“Kamati ya Taifa ya Uwekezaji”
 - (b) kwa kufuta ibara ndogo ya (1);
 - (c) kwa kubadili mpangilio wa ibara ndogo za (2) hadi (5) kuwa ibara ndogo za (1) hadi (4) mtawalia; na
 - (d) katika ibara ndogo ya (1) kama ilivyobadilishwa kwa-
 - (i) kuongeza mara baada ya aya (c) aya ifuatayo:
“(d) Waziri mwenye dhamana ya mambo ya nje;” na



- (ii) kubadili mpangilio wa aya (d) hadi (l) kuwa aya (e) hadi (m);
- F:** Katika Ibara ya 6(1) kwa kufuta maneno “kitawasaidia wawekezaji wote, ikiwa ni pamoja na wale ambao hawafungwi na masharti Sheria hii” yaliyopo katika aya ya (f) na badala yake kuweka maneno “kitawahudumia wawekezaji wote, ikiwa ni pamoja na wale ambao hawafungwi na masharti Sheria hii, na kuwasaidia”;
- G:** Katika Ibara ya 9(4) kwa kufuta aya (b) na (c) na badala yake kuweka aya ifuatayo: “(b) wajumbe wengine - miaka mitatu.”;
- H:** Katika Ibara ya 18(4) kwa kufuta maneno “kumi na nne” na badala yake kuweka neno “saba”;
- I:** Katika Ibara ya 19(3) kwa kuongeza maneno “au kipinde kingine chochote kitakachoainishwa kwa biashara ambayo haijatimiza miaka mitatu tangu kuanzishwa” mara baada ya neno “iliyopita” lililopo mwishoni mwa aya (c);
- J:** Katika Ibara ya 20(3) kwa-
 - (a) kuongeza aya ifuatayo mara baada ya aya (c):
 - “(d) mmiliki wa cheti ameshindwa kutimiza wajibu ulioainishwa katika kifungu cha 26;”; na
 - (b) kubadili mpangilio wa aya (d) na (e) kuwa aya (e) na (f) mtawalia;
- K:** Katika Ibara ya 22(2) kwa-
 - (a) kufuta aya (d); na
 - (b) kubadili mpangilio wa aya (e) na (f) kuwa aya (d) na (e);
- L:** Katika Ibara ya 23(2)(a) kwa kufuta neno “mzawa” lililopo katika aya ndogo ya (i) na badala yake kuweka neno “Mtanzania”; na
- M:** Katika Ibara ya 34(3) kwa kufuta maneno “isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili” na badala yake kuweka maneno “isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miezi kumi na mbili”.

Dodoma,
....., 2022

AKK
WUVB